**MWONGOZO WA UWEKAJI ALAMA KWA KISWAHILI**

**SEHEMU YA I: UFAHAMU NA MSAMIATI:(Alama 30)**

**Jibu maswali yafuatayo kuhusu kifungu cha habari kilicho hapa juu.(Alama 20)**

**1. Mzungumzaji katika kifungu hiki ni nani?**
A. Waziri wa elimu
B. Afisa wa elimu katika Mkoa wa Kusini
C. Mwalimu mkuu wa shule
D. Mwananchi mzalendo

**Jibu:** B

**2. Elimu, kwa mujibu wa kifungu, ni nini?**
A. Mafunzo yanayotolewa shuleni pekee
B. Maarifa yanayotolewa na serikali
C. Mafunzo yanayotolewa na jamii darasani au nje ya darasa
D. Kusoma na kuandika tu

**Jibu:** C

**3. Kabla ya mfumo wa elimu kuanzishwa, maarifa yalipitishwaje?**
A. Kupitia vitabu
B. Kupitia redio na televisheni
C. Kupitia masimulizi ya nyanya na mababu
D. Kupitia walimu wa shule

**Jibu:** C

**4. Yafuatayo ni moja ya manufaa ya elimu isipokuwa:**
A. Kupata ajira
B. Kuongeza mapato ya nchi
C. Kuendeleza uhalifu
D. Kuboresha biashara

**Jibu:** C

**5. Mradi wa 'elimu ya gumbaru' ulianzishwa kwa ajili ya nani?**
A. Watoto wa shule ya msingi
B. Walimu wakuu
C. Watu wazima wanaotaka kujifunza kusoma na kuandika
D. Wanafunzi wa vyuo vikuu

**Jibu:** C

**6. Elimu humwezesha mtu kupata ajira ambayo humsaidia:**
A. Kusafiri nje ya nchi
B. Kupata mahitaji ya kimsingi
C. Kuwa tajiri haraka
D. Kuwa kiongozi wa dunia

**Jibu:** B

**7. Mtu asiyeelimika hukumbwa na tatizo gani?**
A. Kupata marafiki wengi
B. Kusoma magazeti kila siku
C. Kushiriki kwa mafanikio katika biashara
D. Kushindwa kusoma na kuandika

**Jibu:** D

**8. Kutopata ajira kunaweza kusababisha baadhi ya watu:**
A. Kuanzisha kampuni kubwa
B. Kujiingiza katika uhalifu
C. Kusafiri nje ya nchi
D. Kuwa walimu

**Jibu:** B

**9. Elimu husaidiaje katika biashara?**
A. Hufanya biashara kufungwa
B. Huwezesha kuendesha mitambo na kufanya hesabu vizuri
C. Hupunguza wateja
D. Hufanya watu wawe maskini

**Jibu:** B

**10. Kwa mujibu wa mzungumzaji, elimu ni nini katika maendeleo?**
A. Msingi wa matatizo
B. Ufunguo wa maendeleo
C. Sababu ya umaskini
D. Mwisho wa maisha

**Jibu:** B

**11.Oanisha maneno katika Sehemu A na maana zake katika Sehemu B.(Alama 10)**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| A. Ajira | **2.** Kazi anayofanya mtu ili kupata mshahara |
| B. Maskini | 3.Mtu asiye na mali au fedha za kutosha |
| C. Teknolojia | 5.Matumizi ya vifaa vya kisasa kurahisisha kazi |
| D. Mawasiliano | 1.Njia ya kupashana habari au kuwasiliana |
| E. Methali | 4.Semi fupi yenye hekima |

**SEHEMU YA II:SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA(Alama30)**

**12.Weka sentensi zifuatazo katika hali kanushi(Alama 5)**

a).Mimi ninapenda masomo.

**=Mimi sipendi masomo.**

b).Mvumilivu hula mbivu.

**=Mvumilivu hali mbivu.**

c)wazee walikumbuka ujana wao.

**=Wazee hawakukumbuka ujana wao.**

d).Simama hapa.

**=Usisimame hapa**.

e).Tungesoma,tungejua mengi.

**=Tusingesoma,tusingejua mengi.**

**13.Chunguza mafungu ya maneno yafuatayo kisha ainisha iwapo ni sentensi au kirai. Alama 5**

1.Sentensi

2. Kirai

3. Sentensi

4. Kirai

5. Kirai

**14.Andika sentensi zifuatazo katika umoja ama wingi.(Alama 10)**

1. Majengo yapi makubwa?

2. Papai lipi limeiva?

3. Nikupe magunia mangapi?

4. Shirika gani linasaidia wakulima?

5. Sasa ninyi mnataka niwape majembe yapi?

**15.kamilisheni sentensi zifuatazo kwa kutumia neno linaloingiza mlingano au tashbiha au mshabaha: (Alama 5)**

1.Mganga anayeshughulikia mambo ka kuboresha uzazi ni mrefu kama twiga / jini / mlingoti.

2.Kiranja wa darasa letu ni mfupi kama kinu.

3.Dadake aliyeambukizwa UKIMWI amekonda na kuwa kama sindano / mbu.

4.Yeye anasema kama kasuku.

5.Kiongozi anayeshughulikia mambo ya uzalishaji mali ana akili kama mchwa.

**16.Geuza sentensi hizi katika usemi wa taarifa (Alama 5).**

1.“Wewe ni mwalimu?” Mtoto aliuliza.

=Mtoto alitaka kujua ikiwa yeye alikua mwalimu .

2“Utafanya ripoti ya mkutano lini?” Mwenyekiti alitaka kujua.

=Mwenyekiti alitaka kujua wakati angefanya mkutano .

3. “Utaenda shuleni lini?” Mama aliuliza .

=Mama alitaka kujua wakati angeenda shuleni .

4 “Kwa nini ripoti ya kifedha haijaonekana?” Katibu mtendaji aliuliza.

= Katibu mtendaji alitaka kujua sababu ya ripoti ya kifedha kutoonekana.

5. “Mlichagua mada gani?” Mwalimu alitaka kujua.

= Mwalimu alitaka kujua mada waliyochagua

**SEHEMU YA III: FASIHI (ALAMA 30)**

**17.FASIHI Shairi kuhusu umuhimu wa Jembe (Alama10)**

1. Mishororo ishirini

2. Vina vya kati ni ‘ka’ na ‘la’. Vina vya mwisho ni ‘ma’ na ‘nga’.

3. Kifaa muhimu kwa wakulima kinachotumiwa katika kutayarisha mashamba kwa upanzi.

4. Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga.

5. a) Mbinu ya mazida - tunausema

b) Mbinu ya inkisari - usende

6. Mizani 320

7. Shairi linalisifu jembe pamoja na kulitia moyo wa kuzidi kufanya kazi. Mtunzi wa shairi analisihi jembe kutochoka katika utendakazi wake kwa wakati wowote ule. Pia, analiombea jembe maisha marefu na yasiyo na vikwazo. (Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi).

8. Ubeti wa kwanza ulisihi jembe limfariji mtunzi wa shairi hili ili naye aliweke liishi zaidi. Hii ni kwa sababu jembe ni kifaa muhimu ambacho kinaenziwa na watu wengi. Jembe ni chanzo cha kipato kwa watu wote na limekuwepo tangu zamani.

**18Tegua vitendawili vifuatavyo:(Alama5)**

1.Askari mlangoni / Kufuri

2. Mhuni wa ulimwengu / Nyuki

3.Mfalme katoa jicho jekundu / Jua linapochomoza

4.Nanywa supu nyama naitupa / Muwa

5.Mzungu anachungulia dirishani / Kamasi

**19.Chagua jibu bora kuhusu maswali mbalimbali ya fasihi (Alama 5)**

**1. Ni ipi kati ya hizi ni tanzu ya fasihi simulizi?**

A. Riwaya

B. Tamthilia

C. Methali

D. Insha

**Jibu:** C

**2. Tamthilia huandikwa kwa lengo la:**

A. Kusomwa kimyakimya tu
B. Kuimbwa
C. Kuigizwa jukwaani
D. Kuhifadhi kumbukumbu

**Jibu:** C

**3. Ni ipi kati ya hizi ni sifa ya mashairi ya kimapokeo?**

A. Hayana vina
B. Hayana mizani
C. Hufuata urari wa vina na mizani
D. Huandikwa kwa lugha ya kigeni

**Jibu:** C

**4. Riwaya ni kazi ya fasihi inayosimulia:**

A. Hadithi ndefu ya kubuni au ya kweli
B. Mashairi mafupi
C. Methali na nahau
D. Nyimbo za jadi

**Jibu:** A

**5. Lengo kuu la fasihi katika jamii ni:**

A. Kuburudisha pekee
B. Kukuza uchumi
C. Kuelimisha, kuburudisha na kukosoa jamii
D. Kufundisha hesabu

**Jibu:** C

**20.Chagua maana bora ya methali zifuatazo:(Alama 5)**

**1. Methali: "Haraka haraka haina baraka." Ina maana gani?**
A. Kufanya mambo kwa polepole ni kupoteza muda
B. Kufanya mambo kwa pupa husababisha makosa
C. Haraka huleta mafanikio
D. Baraka hupatikana kwa kukimbia

**Jibu sahihi:** B

**2. Methali: "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu." Inafundisha nini?**
A. Kila mtu ana haki ya kufanya anachotaka
B. Kusikiliza ushauri ni muhimu ili kuepuka matatizo
C. Wakubwa huwa wanakosea
D. Miguu huvunjika kwa ajali tu

**Jibu sahihi:** B

**3. Methali: "Mtaka cha mvunguni sharti ainame." Ina maana gani?**
A. Lazima ulale chini ili ufanikiwe
B. Kufanikiwa kunahitaji juhudi na kujitolea
C. Kuinama ni ishara ya udhaifu
D. Mvungu ni sehemu ya kupumzika

**Jibu sahihi:** B

**4. Methali: "Bandu bandu humaliza gogo." Inasisitiza nini?**
A. Kushirikiana ni muhimu
B. Kukata mti ni kazi rahisi
C. Kidogo kidogo huleta mafanikio makubwa
D. Gogo haliwezi kumalizika

**Jibu sahihi:** C

**5. Methali: "Samaki mkunje angali mbichi." Maana yake ni ipi?**
A. Samaki huliwa akiwa mbichi
B. Malezi na mafunzo huanza mapema
C. Kupika samaki ni kazi rahisi
D. Samaki ni chakula bora

**Jibu sahihi:** B

21. 21.Riwaya ya**"**Adili na Nduguze'' a)iliandikwa na nani?**(Alama 1**)

= **Adili na Nduguze** ni kazi ya fasihi iliyoandikwa na **Shaaban Robert**

b). b).Toa muhtasari wa riwaya hiyo katika misitari kumi( **Alama 4)**

Muhtasari wa **Adili na Nduguze** katika mistari 10:

Hadithi hii inaeleza maisha ya **Adili** na ndugu zake wawili ambao wanatofautiana katika tabia; Adili ni mwadilifu na mwenye haki, wakati ndugu zake wawili ni wenye tamaa na uovu. Adili, baada ya kurithi urithi kutoka kwa baba yao, anafaidika na mali kwa bidii na busara, lakini ndugu zake wanapoteza mali zao kutokana na ubinafsi na udhaifu wao. Japo Adili anajaribu kuwasaidia ndugu zake, mara nyingine wanamdhihaki na kumkabili vibaya. Kati ya mambo ya ajabu ni vilumbe vya kishujaa vinavyoonekana kama sehemu ya uwepo wa mafundisho na ushahidi wa adili dhidi ya uovu.

Hatimaye, kazi hii inatoa funzo la kina juu ya uadilifu, haki, na adhabu kwa wale wanaojihusisha na tamaa na tabia mbaya.

(Mwalimu aelewe hoja za mwanafuzi kwa sababu kuna hoja nyingine vile vile na utungaji)

**SEHEMU YA IV:UTUNGAJI(Alama 10)**

**22.Katika mada mbili zifuatazo , chagua mada moja:**

a).Tunga insha kati ya maneno 200 na 250 kuhusu mada: Athari za Matumizi Mabaya ya Mitandao ya Kijamii kwa Vijana

**Jibu**

Matumizi ya mitandao ya kijamii yameongezeka sana katika miaka ya hivi karibuni, hasa miongoni mwa vijana. Mitandao kama Facebook, Instagram, TikTok na X imekuwa sehemu ya maisha ya kila siku. Ingawa mitandao hii ina faida kama kuwasiliana na kujifunza, matumizi mabaya yanaweza kuwa na athari kubwa kwa vijana.

Kwanza, matumizi kupita kiasi husababisha kupoteza muda na kushuka kwa kiwango cha masomo. Vijana wengi hutumia saa nyingi mtandaoni badala ya kusoma au kushiriki shughuli za maendeleo. Pili, mitandao inaweza kuathiri afya ya akili. Ulinganisho wa maisha yao na yale wanayoona mtandaoni unaweza kusababisha msongo wa mawazo, wivu, na kupungua kwa kujiamini.

Aidha, matumizi mabaya yanaweza kusababisha uraibu. Vijana hujikuta wakishindwa kuacha kutumia simu au kompyuta, jambo linaloathiri usingizi na mahusiano yao na familia. Pia kuna hatari ya kukumbana na maudhui yasiyofaa au watu wenye nia mbaya, hali inayoweza kuhatarisha usalama wao.

Kwa hiyo, ni muhimu kwa vijana kutumia mitandao ya kijamii kwa kiasi na kwa malengo chanya. Elimu juu ya matumizi salama ya mitandao pamoja na usimamizi wa wazazi na walimu inaweza kusaidia kupunguza athari hizi na kuhakikisha vijana wananufaika badala ya kuathirika.

b). Wewe ni mwanafunzi wa Kidato cha Sita katika Shule ya Sekondari ya Mwanga. Andika barua kwa Mkuu wa Shule ukiomba ruhusa ya kutokuwepo shuleni kwa muda wa siku tatu kwa sababu ya kuhudhuria mazishi ya babu yako yaliyofanyika kijijini.

**Jibu**

Shule ya Sekondari ya Mwanga,
S. L. P. 45,
Songea.
26 Februari 2026.

Kwa Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari ya Mwanga,
S. L. P. 45,
Songea.

YAH: OMBI LA RUHUSA YA SIKU TATU

Mheshimiwa Mkuu wa Shule,

Husika na kichwa cha habari tajwa hapo juu. Mimi ni mwanafunzi wa Kidato cha Sita katika shule hii. Naandika barua hii kukuomba ruhusa ya kutokuwepo shuleni kwa muda wa siku tatu kuanzia tarehe 27 Februari hadi 1 Machi 2026.

Sababu ya kuomba ruhusa hii ni kwamba ninatarajia kusafiri kwenda kijijini kuhudhuria mazishi ya babu yangu mpendwa yaliyopangwa kufanyika tarehe 28 Februari 2026. Ni wajibu wangu kushiriki pamoja na familia katika kipindi hiki cha maombolezo.

Naahidi nitakaporudi nitaendelea na masomo kama kawaida na nitahakikisha napata maelezo yote niliyokosa darasani.

Naomba ruhusa yangu ikubaliwe.

Wako mtiifu,

JINA
Kidato cha Sita.

**Bahati Njema!!!!**